


# Eastern Africa Journal of Kiswahili

[ISSN 2958-1036]
Volume: 04 Issue: 01 | October-2022

EAJK

# Umuhimu wa Mafumbo Yanayotumika katika Miktadha ya Wosia wa Babu kwa Wavulana Miongoni mwa Wabukusu wa Kenya

**Authors**

**John Swala Barasa Wangila [1]; Wandera-Simwa, Sheila [2]; Onyango J. Ogola [3]**

**Main author email: johnnswala@gmail.com**

**(1.2.3) Laikipia University, Kenya.**

**Cite this article in APA**

Wangila, J. S. B., Wandera, S. S., & Onyango, J. O. (2022). Umuhimu wa mafumbo yanayotumika katika miktadha ya wosia wa babu kwa wavulana miongoni mwa wabukusu wa kenya. *Eastern Africa journal of Kiswahili*, *4*(1), 69-75. https://doi.org/10.51317/eajk.v4i1.269

OPEN ACCESS A publication of Editon Consortium Publishing (online)

**Article history**
Received: 25.06.2022
Accepted: 05.07.2022
Published: 07.10.2022

Scan this QR to read the paper online

**Copyright**: ©2022 by the author(s). This article is an Open Access article distributed under the terms and conditions of the Creative Commons Attribution-NonCommercial-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-NC-SA 4.0).

**Ikisiri**

Utafiti huu ulihakiki umuhimu wa mafumbo yanayotumiwa katika miktadha ya wosia wa babu kwa wavulana miongoni mwa Wabukusu wa Kenya. Mafumbo ni kipera cha semi katika fasihi simulizi. Tafiti za awali zilijikita katika kipengele cha mafumbo zikishughulikia maudhui na fani ya lugha kwa jumla, lakini bado kuna haja ya kuhakiki umuhimu wa mafumbo yanayotumiwa katika wosia wa babu kwa wavulana katika jamii ya Wabukusu. Hii ndiyo sababu kuu iliyochochea utafiti huu kufanywa ili kulijaza pengo hili la kiusomi. Nadharia ya uamilifu ilitumiwa katika uwasilishaji na uchanganuzi wa data. Kata mbili za Kimilili na Kamukuywa ndizo zilizochaguliwa kuwakilisha kaunti ndogo ya Kimilili. Mbinu za mahojiano na uchunzaji wa kushiriki zilitumika katika ukusanyaji wa data. Utafiti huu ulitumia muundo wa kimaelezo katika kuchanganua na kuwasilisha data. Sampuli ya kimaksudi ilitumiwa kuchagua wazee wanne wa kati ya miaka sitini na sabini na wavulana wanne wa kati ya miaka kumi na nane hadi ishirini na mbili kutoka kila kata husika ili kushiriki katika utafiti. Ilibainika kuwa babu hutumia mafumbo kuficha siri, kushauri, kuonya, kuleta utangamano, kuhimiza ubunifu, kukuza lugha, kukuza maadili mema na kupunguza makali katika semi miongoni mwa wavulana. Utafiti huu utatumiwa kama marejeleo na wasomi wengine katika tafiti zinazohusu jamii ya Wabukusu.

**Maneno muhimu**: Uamilifu, muktadha, tohara.

**UTANGULIZI**

Fasihi simulizi imegawika katika tanzu kama vile utanzu wa hadithi, utanzu wa semi, utanzu wa mazungumzo, utanzu wa maigizo, utanzu wa nyimbo au ushairi simulizi na utanzu wa ngomezi (Murimi et al, 2016). Utanzu wa semi una vipera kama vile lugha ya mafumbo, methali, nahau na misemo (Mulokozi, 1989). Kwa hivyo mafumbo ni kipera cha semi katika fasihi simulizi. Wosia ni mawaidha yanayotolewa kwa wavulana katika sherehe mahsusi ya Wabukusu ambayo hutekelezwa katika miktadha ya miviga ya Wabukusu. Katika mawaidha haya babu hutumia lugha ya mafumbo.

**MAPITIO YA MAANDISHI**

Misiko (2017) alionyesha kuwa utamaduni wa jamii ya Wabukusu hupitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine kwa kutumia lugha fiche yaani mafumbo. Wosia wenye mafumbo haya hutolewa katika sherehe za tohara katika jamii hii. Sherehe hizi hutumiwa kwa sababu ndio fursa nzuri ya kuwapata wanajamii wakiwa pamoja. Wazee hutumia mafumbo kupitisha maudhui, dhamira mbali mbali na kuonyesha umahiri wao katika umilisi wa fani za lugha. Utafiti wa Kyabalishanga (2018) ulionyesha kuwa mafumbo katika methali hutumiwa ili kuficha na kupunguza makali ya maneno hasa yale ambayo hayafai kutamkwa mbele ya watu wenye heshima na watoto wadogo. Kwa mujibu wa utafiti wake, wanajamii ya Kihaya hutumia mafumbo ili kudumisha mila na desturi za jamii yao. Mafumbo hutumiwa kama nguo katika semi ili kupoza moto unaowaka. Kulingana na utafiti wa Silau (2013) nyimbo nyingi za ngoma katika jamii ya Wakaguru hutumia mafumbo ili kuficha maneno fulani kwa wasiohusika ili yaeleweke tu na wale wanaohusika. Hii inamaanisha nyimbo hizi hutumia mafumbo ili kuficha siri za jamii hii zisitoke nje na kujulikana na watu wengine.

**Nadharia ya Uamilifu**

Nyonje (2006) anaihusisha nadharia ya uamilifu na Evans Pritchard na Radcliffe Brown. Kwa mujibu wa Namanya (2015), nadharia ya uamilifu iliasisiwa na Auguste Comte, Herbert Spencer, Vilfredo na Emile Durkheim. Hamza (2013) anadai kuwa kila kitu duniani kina mfumo wenye vijisemu ambapo kila kijisehemu kina kazi yake mahususi. Hali hii pia inalinganishwa na mwili wa binadamu ambao una sehemu nyingi. Hii ni sawa na fasihi ambayo ina tanzu na vipera vyake ambapo kila kipera huwa na umuhimu katika jamii. Kwa hivyo, fasihi simulizi huwa na lengo la kuleta ujumbe fulani katika jamii husika. Kwa kuzingatia haya, mafumbo kama kipengele cha fasihi simulizi huwa na lengo fulani katika jamii. Makala hii ilitumia kipengele cha nadharia ya uamilifu kinachodai kuwa kila kijisehemu au utanzu wa fasihi huwa na jukumu mahususi kwa kushirikiana na vijisehemu vingine katika mfumo wa kitu hicho ili kutathmini umuhimu wa mafumbo yanayotumika katika miktadha ya wosia wa babu kwa wavulana miongoni mwa Wabukusu wa Kenya.

**MATOKEO**

**Umuhimu wa Mafumbo**

**Kuficha Siri**

Misiko (2017) anadai kuwa tamaduni za Wabukusu hupitishwa kwa wavulana kwa njia fiche. Yeye anatoa mifano ya mafumbo yanayopatikana katika jamii ya Wabukusu kama vile *kuchomwa na ukwe na mlango uliofungwa.* Haya ni miongoni mwa mafumbo ambayo hutumiwa na wazee kuwapa wavulana ushauri. Katika wosia wao, babu hutumia mafumbo ili kuficha siri katika jamii hii. Jamii hii huamini kuwa lugha ya Kibukusu ni fumbo kwa sababu watu kutoka makabila mengine hawaelewi lugha hii. Kwa hivyo chochote ambacho husemwa katika lugha ya Kibukusu hubaki kuwa siri miongoni mwa wanajamii. Katika hali hii, Wabukusu wakitaka kuficha siri zao kwa mtu kutoka kabila jingine huzungumza kwa lugha ya Kibukusu na kile kisemwacho hakitaeleweka na mtu wa kabila jingine.

Jamii hii kama jamii zingine duniani ina mila na desturi ambazo huwa hawataki zijulikane kwa watu ambao si wanajamii hii au wale walioasi jamii. Hali hii ni sawa na alivyobainisha Mberwa (2015) kuwa waganga hutumia mafumbo ili kuficha hali ya vitisho na ukatili unaoambatana na masuala ya uganga. Anaeleza kuwa waganga pia huficha majina ya miti ya kimatibabu ili isijulikane na watu wengine. Wazee wa jamii ya Wabukusu huwa watu wa heshima katika jamii hii na kuna maneno hawawezi kusema kwa njia ya moja kwa moja mbele ya wavulana. Kuna mambo kama vile sehemu za mwili, matendo ya kingono na mambo mengine ya kinyumba ambayo babu hawaruhusiwi kuyataja mbele ya watu walio na umri mdogo. Kwa

hivyo, wao huficha maneno haya katika mafumbo. Mafumbo hutumiwa kama lugha ya siri katika kupitisha mila na tamaduni kutoka kizazi kimoja hadi kingine.

**Kushauri**

Kupitia kwa mafumbo, wavulana katika jamii ya Wabukusu hushauriwa jinsi ya kuchagua wake wakati wa kuoa ukifika. Wavulana hushauriwa juu ya sifa za mwanamke mzuri ambaye anaweza kuwa mke. Huelezwa kuwa wasiangalie tu maumbile kwani binadamu hudanganya kuwa mzuri kisha kubadilika baadaye. Sifa za mke mzuri hazionekani kwa kuangalia maumbile ya mtu bali hushauriwa kuwa makini kwa kumsoma mtu kwa undani. Mashauri haya yote hutolewa kwa lugha ya kimafumbo na babu mahususi walioteuliwa na jamii. Kwa mfano;

*Okhaila nafokoyo tawe.*

Tafsiri

*Usioe mke mvivu.*

Hili ni fumbo linalotumiwa kuwaongoza wavulana katika mchakato wa kuchagua wake. Fumbo hili linawashauri wavulana wasioe wake wavivu. Jamii ya Wabukusu huamini kuwa uvivu ndicho chanzo cha umaskini katika jamii.

**Kuonya**

Mafumbo hutumiwa kama maonyo. Wazee katika jamii ya Wabukusu huonya wavulana kwa kutumia mafumbo bila kusema jambo moja kwa moja. Kwa kutumia mafumbo, wazee huwaonya wavulana dhidi ya madawa ya kulevya. Wazee hueleza wavulana kuwa madawa ya kulevya huwa na athari mbaya sana katika maisha na afya ya wavulana. Wao huelezwa kuwa madawa ya kulevya huweza kusababisha ugonjwa wa akili pamoja kusambaratisha familia zao sababu mtu mlevi huwa hakimu mahitaji ya familia yake na huwaacha watoto na mkewe wakiteseka ilhali yeye mwenyewe anajiburudisha katika anasa. Walevi hawa pia huwa hawajielewi, jambo ambalo huweza kusababisha kujiingiza katika vitendo vya kingono nje ya ndoa ambalo ni jambo hatari sana kwa ndoa.

Kupitia kwa mafumbo, wavulana huonywa dhidi ya kupenda anasa kupita kiasi. Wavulana huelezwa kuwa mambo ya kingono huweza kusababishia magonjwa ya zanaa ambayo huwa hatari sana kwa maisha yao na yale ya wake wao ikiwa wameoa. Mafumbo pia hutumiwa kuwaonya wavulana dhidi ya makundi mabaya kwa sababu tabia yaweza kuambukizwa. Wao huambiwa waepuke makundi mabaya ili wasijipate upande mbaya wa sheria. Mafumbo huwaelezea kuwa mtu mwovu akitenda jambo mbaya na ashikwe, marafiki wake pia huusishwa katika jambo hilo na huenda waumie kwa makosa ambayo hawajatenda. Maonyo haya hufanywa kupitia kwa mafumbo kwa sababu huenda yule ambaye wanaonya wavulana kumhusu awe katika kile kikao na wakitumia lugha ya moja kwa moja huenda akasikia na akasirike. Kwa hivyo ili yeyote asijue anasemwa, mafumbo hutumiwa.

Mafumbo huonya dhidi ya uvivu kwa kutumia hadithi zinazoitwa mbazi, yaani hadithi za kimafumbo. Katika hadithi hizi, majina ya wanyama pamoja na tabia zao hutumika ili kuonyesha tabia za binadamu. Majina ya wanyama hutumika ili kuficha tabia ya binadamu kwa sababu watu wakitajwa kwa njia ya moja kwa moja kuna wale ambao wataudhika na kuleta ugomvi katika jamii. Kwa hivyo ili kusiwe na ugomvi wowote, lugha fiche hutumiwa katika maonyo haya. Kwa kutumia majina ya wanyama pamoja na vitu vingine vinavyopatikana katika mazingira, wavulana huonywa dhidi ya ulafi. Wavulana huambiwa kuwa ulafi husababisha matendo mabaya kama vile wizi na unyang'anyi katika jamii. Wavulana huimizwa kutosheka na kile walichobarikiwa nacho hata kama ni kidogo. Wavulana hawa pia huelezwa umuhimu wa kutumia mali yao kwa njia nzuri. Kwa mfano.

*Omwana umulai okhaboa chisilingi khwineke tawe.*

Tafsiri

*Mtoto mzuri usiweke pesa zake kwenye sehemu zako za uume.*

Hili ni fumbo la maonyo. Fumbo hili ni mfano mzuri wa fumbo linalowafunza wavulana jinsi ya kutumia mali yao. Wavulana wanaonywa dhidi ya kutumia mali yao kuwafurahisha makahaba. Wavulana huonywa kuwa makahaba huwapotosha wavulana wengi na kuwa na maisha yasio mazuri.

**Kuwafikirisha Walengwa**

Kulingana na Ayiera (2017), mafumbo hutumia lugha fiche inayombidi msikilizaji kufikiria sana ili apate maana au jibu. Lugha ya kimafumbo huwa si lugha ya moja kwa moja bali ni lugha ambayo humhitaji msikilizaji kufikiria sana ili afahamu maana ya kile kinachosemwa. Hii ni lugha ambayo huhitaji msikilizaji kufikiria na kugonga kichwa sana ili apate jibu. Hii ni

kwa sababu ya lugha fiche inayotumiwa ambayo haieleweki kwa urahisi. Kulingana na utafiti wa Mberwa (2015), wimbo wa *Puuo* hutumia maneno ya kawaida lakini ndani yake huwa na maana nyingine ya ziada. Anaeleza kuwa ili msikilizaji ajue maana ya wimbo huo, itamhitaji kufikiria sana. Katika jamii ya Kasena, Awedoba (2000) anadai kuwa mafumbo huwafanya watoto kufikiria kuhusu mazingira ambamo wenyewe wanatoka. Kwa mfano;

*Namunyu yabolela libale eli wakhasila waulile.*
Tafsiri
*Fisi aliliambia jiwe eti hata ukinyamaza umesikia.*

Hili ni fumbo ambalo hutumiwa kama hitimisho katika wosia. Fumbo hili huwafanya wavulana kufikiria sana kuhusu yale yaliyosemwa. Fumbo hili huwa kama taharuki katika wosia. Taharuki hii ndiyo huwafikirisha walengwa.

Mafumbo hutumiwa katika wosia katika jamii ya Wabukusu kuwafanya wavulana kufikiria kuhusu masuala mbalimbali katika jamii hasa maisha yao ya ukomavu watakapokuwa wazazi na viongozi wa familia zao. Wavulana wanapofikiria sana na kukosa majibu, huwa funzo kwao kwani wao huelewa kuwa maisha yana changamoto na huhitaji umakini ili kushinda changamoto hizo. Mara nyingi wavulana wanaposhindwa kupata maana au majibu ya mafumbo haya, wao huwaelezea babu au wazee fulani ili wawaelezee maana. Wazee huwa hawatoi maana au jibu la moja kwa moja bali hudokeza tu ili wavulana waendelee kufikiria tena. Wazee huamini kuwa wavulana wakipewa maana au majibu ya mafumbo kwa njia ya moja kwa moja, huonekana kuwa wanawawafanyia maisha kuwa rahisi na huenda wateseke ikiwa watapatikana katika shida na pasiwe na mzee au mtu wa kuwasaidia. Wao huwataka wavulana wafikirie wenyewe ili wawe na uwezo wa kujifanyia mambo wenyewe ili wasitegemee msaada kila mara. Jukumu la wazee huwa kuelekeza wavulana katika masuala mbalimbali ya maisha na sio kuwafanyia majukumu yao wenyewe. Kufikiria wenyewe huwafanya wavulana kuwa wajibikaji na sio tu kutegemea msaada kutoka kwa watu wengine.

**Kuhimiza Utangamano Katika Jamii**

Mafumbo huwaleta wanajamii pamoja ili kushiriki vikao vya mafumbo. Vikao vya wosia katika jamii ya Wabukusu ambapo lugha ya mafumbo hutumiwa huhudhuriwa na wavulana wengi ambapo ushirikiano huhimizwa. Sherehe za kuwapa wavulana wosia katika jamii ya Wabukusu huwavutia watu wengi kwa sababu lugha inyotumika katika sherehe hizi huwa ya kimafumbo na hupendwa na wanajamii wengi. Watu huja pamoja ili wafurahie lugha hii ambapo wao hucheka na kuburudika na lugha hii ya siri.

Kwa upande mwingine, kuna mafumbo ambayo huimiza umoja wa wanajamii katika jamii ya Wabukusu. Mafumbo haya huimiza watu wakija pamoja huweza kufanya mambo mengi makubwa katika jamii. Mfano wa mafumbo kama haya ni kama;

*Babandu kimiantu*
Tafsiri
*Watu ni mali*

Hili ni fumbo linalotumia istiari kama mbinu ya lugha linalosema kuwa watu ni mali. Hii ni kumaanisha kuwa palipo na watu wengi kuna mali. Hata kama watu waliokusanyika mahali fulani ni masikini, wanaweza kuchangia kidogo walichonacho na kuwa na mali nyingi sana. Mafumbo haya huimiza utendakazi kwa pamoja ili kuwa na mali nyingi katika jamii. Mali hii inaweza kuwa mali halisi kama vile ng'ombe, mahindi, mashamba, watoto au hata mali ya akili. Akili nyingi huonekana kama mali kwa sababu watu wakifikiria pamoja huweza kupata suluhisho la haraka kuliko akifikiria mtu mmoja. Hali hii huondoa uadui katika jamii ya Wabukusu na kuhimiza ushirikiano katika kila jambo linalofanwa. Kwa hivyo fumbo hili huimiza umoja katika jamii ya Wabukusu.

**Kukuza Ubunifu Katika Jamii**

Ili babu wapate lugha yoyote ya siri ambayo wanataka kutumia, lazima wawe wabunifu ili kutambua misamiati ya siri ya lugha hiyo. Kwa kawaida mafumbo hutumia lugha ya kawaida lakini maana huwa si ya kawaida inayojulikana katika jamii ya Wabukusu. Ubunifu wa hali ya juu huhitajika ili babu watumie lugha ya kawaida na kutoa maana isiyo ya kawaida, maana fiche. Ili kutoa maana fiche katika misemo inaoonekana kuwa ya kawaida inahitaji ubunifu wa hali ya juu. Maoni haya ni sawa na yale yaliyotolewa na Salim (2018) anapodai kuwa mafumbo katika vitendawili hudhihirisha ubunifu wa wanafasihi. Kwa mfano;

*Babukusu khubitilanga omwana lipanga, lijembe, eshoka, lubereru, lifumo, esimbo nende engabo.*
Tafsiri
*Wabukusu huosia kutumia panga, jembe, shoka, kifwekeo, mkuki, fimbo na ngao.*

Hili ni fumbo ambalo babu katika jamii ya Wabukusu wamebuni vifaa vya kutumia kuwapa wavulana wosia. Vifaa kama vile panga, jembe, shoka, ufyekeo, ngao na fimbo ni vifaa vya kazi lakini babu wamevibuni ili kutoa maana fiche katika wosia.

Sababu ya kutumia mafumbo katika wosia ni kuwahimiza wavulana kubuni mbinu mbalimbali za kutatua matatizo ya kimaisha katika ulimwengu wao. Jinsi wavulana wanavyofikira na kubuni majibu na maana ya mafumbo kutoka kwa wosia wa babu wao, vivyo ndivyo wanastahili kubuni mbinu mbalimbali za kutatua matatizo yanayowakumba katika maisha yao. Mafumbo au lugha fiche inayotumiwa katika wosia, hulinganishwa na matatizo ya kimaisha ambayo wavulana huhitajika kubuni mbinu za kuyatatua. Wavulana huhimizwa kuwa ugumu wanaoupata katika kupata majibu na maana ya mafumbo yanayotolewa katika wosia wanaopewa na babu wao, ndio ugumu uliopo katika kutatua matatizo katika maisha halisi. Kwa sababu maisha huwa na matatizo mengi, wavulana hupewa ujuzi na maarifa ya kutafuta suluhisho kwa matatizo haya.

**Kukuza Lugha**

Kulingana na maoni ya Mberwa (2015), mafumbo hutumiwa kuvisha lugha nguo katika mashairi. Anaeleza kuwa mafumbo hutumiwa katika mashairi kama pambo la lugha ya fasihi. Suala hili ni sawa na mafumbo katika jamii ya Wabukusu ambapo mafumbo haya huendeleza ukuaji na uenezaji wa lugha ya Kibukusu. Ulumbi na ugambizi ni taaluma ambazo huigwa na wanajamii ya Wabukusu. Watu huiga taaluma hii kupitia kwa mazoezi ya mara kwa mara. Mazoezi haya hupatikana kupitia kwa miktadha ambayo babu huwapa wosia wavulana katika hafla mbalimbali kama vile sherehe zinazofanyika baada ya tohara. Katika hafla hizi, mazungumzo husheheni mafumbo yanayonuia kuwazindua wavulana katika matumizi yao ya lugha. Kwa kufanya mazoezi haya ya mazungumzo ya lugha ya kimafumbo, babu huwa weledi katika matumizi ya lugha na hivyo lugha hukua miongoni mwao. Mazungumzo haya pia huimarisha umilisi wa lugha ya Kibukusu.

**Kukuza Maadili Mema**

Katika jamii ya Wabukusu, maadili mema hukuzwa na yale mabaya hukashifiwa kupitia kwa mafumbo yanayotolewa katika Wosia wa babu kwa wavulana wao hasa baada ya kupaswa tohara. Maadili haya hupitishwa katika tamaduni za Wabukusu kwa kuwatumia wazee walioteuliwa katika jamii. Kulingana na utafiti wa Misiko (2017) lugha inayotumiwa katika kupitisha utamaduni wa Wabukusu kutoka kizazi kimoja hadi kingine huwa lugha fiche, yaani lugha ya kimafumbo. Babu hukashifu matendo mabaya kupitia kwa mafumbo kwa sababu matendo mabaya huweza kuwaletea wavulana shida katika maisha yao ya badaaye. Tabia mbaya hukashifiwa kwa sababu huleta ugomvi katika jamii na hufanya wanajamii kuishi bila amani. Baadhi ya mafumbo yanayokashifu matendo mabaya katika jamii ya wabukusu ni kama;

*Okhaba nende kimikhono kitaru tawe*
Tafsiri
*Usiwe na mikono mitatu.*

Hili fumbo ambalo linakashifu wizi. Wizi ni kitendo kibaya miongoni mwa wanajamii na huenda ukiwaletea shida kama vile kupigwa ikiwa watashikwa. Wale wanaotegemea wizi huenda wakawa wavivu kwa sababu wao hupata mali au riziki kwa njia rahisi.

Mafumbo hutumiwa kwa wavulana ili washike mambo vizuri na kuyakumbuka wakati unaostahili. Wavulana kwa mara nyingi wakiambiwa maneno au wakipewa wosia kwa njia ya moja kwa moja huenda wakasahau haraka. Ili wosia wa babu wao ugande katika kumbukizi zao, mafumbo hutumiwa. Njia hii hukuza kumbukizi ya wavulana na utekelezaji wa yale waliyoambiwa na wakubwa wao. Mafumbo huwasaidia wavulana kukumbuka kwa sababu mafumbo hutumia vitu vinavyopatikana katika mazingira yao na wavulana wanapoona vile vitu ambavyo vilitumiwa katika fumbo fulani, wao hukumbuka kile walichoambiwa katika wosia fulani. Babu pia katika jamii ya Wabukusu huwa ni watu walioishi miaka mingi na hao hutoa mafumbo katika wosia wao kwa kutumia tajriba yao. Hivi ni kumaanisha kuwa wao huongea na kutoa mifano kwa kutumia mambo ambayo wao wenyewe wamepitia na kuyaona katika maisha yao.

**Kupunguza Makali katika Semi**

Kuna mambo ambayo yakielezwa au jamii ikiambiwa kwa njia ya moja kwa moja huenda watu wakashtuka sana na hata wengine wenye ugonjwa wa shinikizo la damu wakaaga dunia. Kwa hivyo ujumbe ambao ni wa kushtua huelezwa kwa kutumia lugha ya kimafumbo. Ikiwa kwa mfano jamii imekumbwa na janga kama vile kifo, kuna lugha ambayo wanajamii hupasha ujumbe huu kwa watu walio mbali. Hali hii ni sawa jinsi inavyodhihirishwa na utafiti wa Mberwa (2015) ulioonyesha kuwa waganga hutumia mafumbo ili kuondoa ukali na hofu katika usemi na shughuli za uganga.

Mfano katika jamii ya Wabukusu huwa, ikiwa mamake mtu amefariki na umepewa jukumu la kupeleka ujumbe huu, basi utasema nilimwacha mamako akiwa mgonjwa sana na angependa kuongea na wewe. Mtu huyo anapoambiwa maneno haya hatajua mamake amefariki bali ni mgonjwa tu. Itamchukua mtu huyo muda mrefu kufikiria na kugundua kuwa mama yake ameaga dunia. Katika harakati hiyo hatakuwa na mshtuko sana kama angeambiwa moja kwa moja kuwa mama yake amefariki.

Mafumbo hutumiwa kama nguo katika semi ili kupoza moto unaowaka (Kyabalishanga, 2018). Kuna semi ambazo huwa na ukali fulani na huenda semi hizo ziwe miiko katika jamii au zionyeshe kukeukwa kwa maadili ikiwa zitatajwa waziwazi. Ili kutaja semi hizi, mafumbo hutumiwa. Mafumbo haya hutumiwa kutaja sehemu za siri, matendo ya ngono na hata uhusiano ambao haustahili kutajwa kwa njia wazi. Hii ni sawa na jamii ya Kihaya ambapo Kyabalishanga (2018) anadai kuwa mafumbo hutumiwa katika methali ili kuvisha semi nguo. Jamii ya Wabukusu pia hutumia mafumbo kwenye methali ili kuficha ujumbe fulani. Kwa mfano,

Methali; *Wamwene nokenda bubi onyala wetuya.*

Tafsiri

Methali: *Wewe mwenyewe ukitembea vibaya unawezakujikwaa.*

Maneno ‘kutembea’ na ‘kujikwaa’ yametumiwa kimafumbo katika methali hii. Yanamaanisha kutokuwa makini unavyoishi duniani au unavyofanya mambo yako. Wavulana huhimiswa kuwa makini katika vitendo hatari kama vile mapenzi ya kiholelaholela kwa sababu wanaweza kupata magonjwa ya zinaa kama UKIMWI. Kujiingiza katika mapenzi ya kiholela ndiko ‘kutembea vibaya’ na Kupata magonjwa haya ndiko ‘kujikwaa.’

Methali: *Engokho endai siruchu sasitila binywinywi tawe.*

Tafsiri

Methali: *Kuku mzuri mwewe hashiki vifaranga wake.*

Hii ni methali inayotumia kuku na vifaranga wake ili kuonyesha jinsi kiongozi anastahili kuwalinda watu wake. Katika methali hii, neno’ kuku’ limetumiwa kuonyesha kiongozi na neno vifaranga limetumiwa kuashiria wafuasi wa kiongozi. Methali hii katika jamii ya Wabukusu hutumiwa katika wosia wa babu kwa wavulana kuwashauri kuwa wakiwa viongozi katika nyadhifa zozote, wanastahili kuongoza vyema na kuwalinda watu wao kama kuku anavyolinda vifaranga wake.

**MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

**Mahitimisho**: Ili kutathmini umuhimu wa mafumbo katika miktadha ya wosia wa babu kwa wavulana miongoni mwa jamii ya Wabukusu, mhimili wa nadharia ya uamilifu unaodai kuwa kila kijisehemu au utanzu wa fasihi huwa na jukumu mahususi kwa kushirikiana na vijisehemu vingine katika mfumo wa kitu hicho ulitumiwa. Makala hii ilibainisha kuwa mafumbo kama kijisehemu cha fasihi simulizi yana umuhimu mkubwa katika jamii ya Wabukusu. Ilibainika kuwa mafumbo hutumiwa kuficha siri, kushauri, kuonya, kuleta utangamano, kuhimiza ubunifu, kukuza lugha, kukuza maadili mema, kupunguza makali katika semi, kuhimiza udadisi na kukuza stadi ya kusikiliza miongoni mwa wavulana.

**Mapendekezo:** Serikali za kaunti zitambue umuhimu wa miviga inayolenga kuwapa wavulana wosia kwa njia za kimafumbo na kuzifadhili. Hii ni kwa sababu wanajamii wengine hawaandai sherehe hizi kwa sababu ya ukosefu wa fedha. Sherehe hizi zikipata ufadhili, wavulana wengi watapata mafumbo mengi kutoka kwa wazee na wavulana hao pia watapitisha mafumbo haya kwa vizazi vijavyo. Katika kutathmini umuhimu wa mafumbo yanayotumiwa katika muktadha wa wosia wa babu kwa wavulana, utafiti huu ulijikita katika umuhumu wa mafumbo pekee bila kushughulikia umuhimu wa vipera vingine vya semi vinavyopatikana katika fasihi ya Wabukusu. Kwa hivyo utafiti huu unapendekeza tafiti zingine zifanywe ili

kupambanua umuhimu wa vipera vingine vya semi vinavyopatikana katika jamii ya Wabukusu.

**MAREJELEO**

Awedoba, K. (2000). Social roles of riddles, with reference to kasena society. *African e-Journals.*

Ayiera, E. (2017). *Ufumbaji Katika Riwaya za Katama Mkangi.* Tasnifu ya Uzamili katika Chuo Kikuu cha Maasai Mara.

Hamza, M. (2013). *Kufanana na Kutafautiana kwa Maudhui na Fani Kati ya Methali za Kitanzania na za Kilibya: Utafiti Linganish.* Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Kyabalishanga, F. (2018). *Kuchunguza Sanaa na Dhima za Methali za Wahaya.* Tasnifu ya Uzamili ya Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Mberwa, A. (2015). *Athari ya Matumizi ya Mafumbo na Tamathali za Semi Katika Nyimbo za Ngoma ya Puuo Kwa Wazanzibari*. Tasnifu ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dodoma.

Misiko, D. (2017). *Lugha Kama Rasilimali Ya Jamii: Uchunguzi wa Redio za FM Zinazotumia Kibukusu Katika Kaunti ya Bungoma*. Tasnifu ya Uzamili katika Chuo Kikuu cha Moi.

Mulokozi, M. M. (1989). *Tanzu za Fasihi Simulizi. Katika, Mulika*. Na. 21. Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Murimi, J., Obuchi, S., & Kandagor, M. (2016). Mwingilianotanzu Katika Uainishaji wa Tanzu za Fasihi Simulizi ya Kiswahili. *IJRDO-Journal of Educational Research.*

Namanya, J. (2015). *Dhima ya Misemo na Nahau Katika Jamii ya Wachiga Wilayani Kabale Kusini Mangharibi mwa Uganda*, Tasnifu ya Uzamili katika Chuo Kikuu cha Pwani.

Nyonje, J. W. (2006). *Mwonoulimwengu wa Waswahili Jinsi Unavyojitokeza katika Ngano.* Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Nairobi.

Salim, M. (2018). *Sanaa na Mshikamano wa Maudhui Katika Vitendawili.* Tasnifu ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar.

Silau, G. (2013). *Kutathmini Dhima ya Nyimbo Katika Kukuza na Kuimarisha Malezi, Mfano Wa Kabila La Wakaguru*. Tasnifu Ya Kiswahili ya chuo Kikuu Huria cha Tanzania.